**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**



# JARIDA LA KOROSHO
# MWEZI MACHI, 2023

VOL. 1 CBT.Na.0007

Imeandaliwa na: **BODI YA KOROSHO TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA

## 1.0 UTANGULIZI

Msimu wa Korosho nchini Tanzania unaanza mwezi Oktoba na kuisha mwezi Aprili kila mwaka. Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani msimu wake huisha Januari wakati Tanga, Dodoma na Singida huendelea hadi mwezi April.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi sasa zaidi ya tani 168,971.063 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 155,707,740.67 (FOB Value) zimepatiwa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,641.861 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 50,603,117.97 (FOB Value) zimesafirishwa.

## 2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast, kiasi kikubwa cha korosho kinapelekwa mjini Abidjan, kiasi cha korosho kinachonunuliwa kimeshuka kutokana na kutofautiana kwa bei za ndani na zile za kimataifa. Ubora wa korosho ghafi sio kama ilivyotarajiwa kwani umeshuka kwa kiasi kikubwa. Hadi sasa inakadiriwa kuwa korosho ghafi zilizouzwa zimeshafikia takribani tani 260,000 hadi 280,000 na bei za korosho ni takribani Dola za Kimarekani 1,160 hadi 1,180 (CIF-Vietnam) kwa tani kwa korosho zenye ubora wa “48 lbs”.


Nchini Ghana kumekuwa na ongezeko la usambazaji wa korosho ghafi hasa zinazotoka nchini Ivory Coast na hii imepelekea kupungua kwa bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima. Bei ya sasa ni kati ya Dola za Kimarekani 0.69 hadi 0.73 kwa kilogramu kulingana na kiwango cha unyevu.

Kwa upande wa Benin uzinduzi wa msimu wa korosho ulifanyika tarehe 16 Machi, 2023 huko Natitingou ukihudhuriwa na viongozi wa kisiasa na wataalamu wa sekta hiyo. Shughuli ya ununuzi na usafirishaji kwenda nje ya nchi itaanza Mei 2023.

Nchini Burkina Faso bei za korosho ghafi zinashuka ambapo ni kati ya Dola za Kimarekani 1,050 hadi 1,070 (CIF-India) kwa tani. Bei ya korosho ngazi ya mkulima ni kati ya Dola za Kimarekani 0.53 hadi 0.58 kwa kilogramu katika mabonde ya Cascades na Hauts. Kwa upande wa Kusini Magharibi mwa Bukina Faso bei ya korosho ghafi ni kati ya Dola za Kimarekani 0.66 hadi 0.78 kwa kilogramu.

## Jedwali Na. 1: Usafirishaji wa Korosho Karanga Kwa Nchi za Afrika Kwenda Nchi za Ulaya Hadi Januari 2023.

| USAFIRISHAJI WA KOROSHO KARANGA KWA NCHI ZA AFRIKA KWENDA NCHI ZA ULAYA HADI JANUARI 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI (TANI) | THAMANI (USD 000) |
| 1 | IVORY COAST | 1,717 | 11,105.56 |
| 2 | BURKINA FASO | 353 | 2,399.63 |
| 3 | GHANA | 127 | 731.96 |
| 4 | NIGERIA | 113 | 672.67 |
| 5 | BENIN | 82 | 385.96 |
| 6 | MSUMBIJI | 65 | 491.57 |
| 7 | TANZANIA | 57 | 410.72 |
| 8 | TOGO | 36 | 260.88 |
| 9 | GUINEA BISSAU | 32 | 111.03 |
| 10 | MADAGASCAR | 12 | 88.40 |
| 11 | SENEGAL | 12 | 133.67 |
| | Jumla Kuu | 2,606 | 16,792.05 |





**Chanzo:** Cashewnutinformation

## 2.2. HALI YA SOKO LA KOROSHO NCHINI INDIA

Nchini India mahitaji ya korosho karanga yameendelea kuwa chini katika mauzo ya nje na mauzo ya ndani. Hata hivyo India inapitia kipindi cha uhaba wa korosho zenye ubora wa kiwango cha juu ambazo zinawavutia walaji wengi wa ndani na nje ya India. Korosho za msimu mpya kutoka nchini Ghana zinatarajia kuanza kuingia nchini India ndani ya wiki mbili zijazo. Matarajio hayo yameshusha bei za korosho ghafi mji wa Goa kufikia Dola za Kimarekani 1.542 kwa kilo huku Maharashtra zikiuzwa Dola za Kimarekani 1.55 kwa kilo (Ex warehouse).

## Jedwali Na.2: Korosho Ghafi Zilizoingia India Kutoka Nchi Mbalimbali hadi Januari 2023.


| KOROSHO GHAFI ZILIZOINGIA INDIA KUTOKA NCHI MBALIMBALI HADI JANUARI 2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI (TANI) | THAMANI (USD 000000) | WASTANI (USD/TANI) |
| 1 | TANZANIA | 38,726 | 53.97 | 1,372 |
| 2 | BENIN | 2,313 | 2.42 | 1,103 |
| 3 | IVORY COAST | 1,998 | 2.16 | 1,117 |
| 4 | GUINEA BISSAU | 1,656 | 2.45 | 1,479 |
| 5 | GUINEA | 1,105 | 1.03 | 914 |
| 6 | BURKINA FASO | 738 | 0.75 | 1,020 |
| 7 | SENEGAL | 634 | 0.74 | 1,139 |
| 8 | UMOJA WA FALME ZA KIARABU | 619 | 0.72 | 1,159 |
| 9 | SINGAPORE | 483 | 0.68 | 1,410 |
| 10 | GHANA | 391 | 0.28 | 626 |
| 11 | NIGERIA | 305 | 0.30 | 1,004 |
| 12 | GAMBIA | 181 | 0.21 | 1,201 |
| 13 | MALAYSIA | 109 | 0.15 | 1,421 |
| 14 | TOGO | 50 | 0.05 | 951 |
| 15 | THAILAND | 44 | 0.05 | 1,223 |
| | Jumla Kuu | 49,352 | 65.96 | 1,337 |




**Chanzo:** Cashewnutinformation

## Jedwali Na. 3: Usafirishaji wa Korosho Karanga India Kwenda Nchi Mbalimbali hadi Januari 2023.

| USAFIRISHWAJI WA KOROSHO KARANGA INDIA KWENDA NCHI MBALIMBALI HADI JANUARI 2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | NCHI | KIASI(TANI) | THAMANI (USD 000000) | WASTANI USD/TANI |
| 1 | UMOJA WA FALME ZA KIARABU | 1,941 | 14.04 | 7,148 |
| 2 | SAUDI ARABIA | 492 | 3.61 | 7,475 |
| 3 | UHOLANZI | 365 | 2.46 | 6,854 |
| 4 | UHISPANIA | 238 | 2.01 | 8,527 |
| 5 | MAREKANI | 175 | 1.37 | 8,834 |
| 6 | QATAR | 106 | 0.79 | 7,326 |
| 7 | OMAN | 90 | 0.61 | 6,595 |
| 8 | AFRIKA YA KUSINI | 25 | 0.20 | 7,859 |
| 9 | SINGAPORE | 16 | 0.12 | 6,739 |
| 10 | USWISI | 8 | 0.08 | 9,754 |
| 11 | UINGEREZA | 4 | 0.03 | 7,602 |
| 12 | NEPAL | 2 | 0.01 | 5,495 |
| | Jumla kuu | 3,462 | 25.33 | 7,464 |





**Chanzo:** Cashewnutinformation

## 2.3. HALI YA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI YA VIETNAM

Nchini Vietnam bei ya korosho ghafi kutoka Afrika zinashuka ikilinganishwa na wiki chache zilizopita. Kwa mwaka huu Vietnam haijanunua kiasi kikubwa cha korosho ghafi kutoka Nigeria hasa kutoka Ogbomosho, hii imetokana na kushuka kwa kiwango cha ubora. Mahitaji ya korosho karanga bado ni kidogo na bei imeshuka ambapo daraja la W320 zinauzwa kwa Dola za Kimarekani 5.40 hadi 5.51 kwa kilo kutoka kwa wabanguaji wa kati na Dola za Kimarekani 5.73 hadi 5.84 kwa kilo kutoka kwa wabanguaji wakubwa.

## Jedwali Na.4: Bei za Korosho Ghafi katika Nchi ya India na Vietnam Machi, 2023

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI (RCN) DUNIANI-CASE STUDY YA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA OKTOBA, 2022 HADI FEBRUARI, 2023 | | |
|---|---|---|
| TAREHE | BEI-CIF USD/TON | |
| | BEI YA CHINI | BEI YA JUU |
| 02 Oktoba, 2022 | 1,080 | 1,350 |
| 31 Oktoba, 2022 | 1,050 | 1,280 |
| 05 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 27 Novemba, 2022 | 1,100 | 1,400 |
| 12 Desemba, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| 24 Desemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 14 Januari, 2023 | 1,200 | 1,275 |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,390 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| SOT: 48-52 | | |




**Chanzo:** Cashewnutinformation

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI mbalimbali

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM MACHI, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ukilinganisha na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko madogo ya bei kwa mwezi Machi kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA MACHI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | WW180 | 7.28 | 8.27 | 16,904.16 | 19,202.94 |
| White Whole Cashews 210 | WW210 | 6.83 | 7.50 | 15,859.26 | 17,415.00 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.84 | 6.40 | 13,560.48 | 14,860.80 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.40 | 5.84 | 12,538.80 | 13,560.48 |
| Large Pieces | LP | 3.19 | 3.86 | 7,407.18 | 8,962.92 |
| Small Pieces | SP | 2.65 | 2.87 | 6,153.30 | 6,664.14 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 BEI YA KOROSHO KARANGA KATIKA NCHI ZA AFRIKA MAGHARIBI MACHI, 2023.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni pamoja na Ivory Coast, Ghana na Benin inakadiriwa kuwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 6**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA MACHI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | | | | |
| White Whole Cashews 210 | W210 | 8.16 | 8.49 | 18,947.52 | 19,713.78 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.95 | 6.17 | 13,815.90 | 14,326.74 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.62 | 5.95 | 13,049.64 | 13,815.90 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.30 | 5.62 | 12,306.60 | 13,049.64 |
| White Splits | WS | 4.41 | 4.74 | 10,240.02 | 11,006.28 |
| Large Pieces | LP | 3.86 | 4.29 | 8,962.92 | 9,961.38 |
| Small Pieces | SP | 3.09 | 3.42 | 7,174.98 | 7,941.24 |

**Chanzo:** Cashewinformation

## 3.3 BEI YA KOROSHO KARANGA ZA TANZANIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI MACHI, 2023

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni nk. Ni kama ilivyo katika jedwali Na. 7

### Jedwali Na. 7

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA MACHI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | W180 | 7.97 | 8.37 | 18,486.00 | 19,422.00 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 7.36 | 7.56 | 17,082.00 | 17,550.00 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 6.96 | 7.26 | 16,146.00 | 16,848.00 |
| White Splits | WS | 3.93 | 4.54 | 9,126.00 | 10,530.00 |
| Large White Pieces | LWP | 3.93 | 4.54 | 9,126.00 | 10,530.00 |

**Chanzo:** TACP

### Jedwali Namba 8: Uwiano wa Bei kwa Korosho Karanga Daraja WW320

| UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nchi | Bei ya Chini Dola/Kilo | Bei ya Juu Dola/Kilo | Bei ya Chini Tzs/Kilo | Bei ya Juu Tzs/Kilo |
| Vietnam | 5.40 | 5.84 | 12,538.80 | 13,560.48 |
| Afrika Magharibi | 5.62 | 5.95 | 13,049.64 | 13,815.90 |
| Tanzania | 6.96 | 7.26 | 16,146.00 | 16,848.00 |

**Chanzo:Bodi ya Korosho**

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2022/2023 ni tani 187,360.022 zenye thamani ya shilingi 343,220,746,595 ambapo tani 176,686.889 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 328,264,230,845. Mwezi Machi bei imeshuka kwa asilimia 1.8 kutoka shilingi 1751 mwezi Februari hadi 1720 mwezi Machi, 2023. Mauzo ya korosho ghafi kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi wa Machi ni tani 4,370.392 zenye thamani ya shilingi 7,380,086,250 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni tani 6,302.741 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 7,576,429,500. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji bado unaendelea.

## Jedwali Na. 9a: Taarifa ya Uzalishaji Korosho Msimu wa 2022/2023 Hadi Kufikia Mwezi Machi, 2023

| TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA TAREHE 31/03/2023 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SN | MKOA | CHAMA KIKUU | GHALA ZA MNADA (KG) | THAMANI GHALA ZA MNADA (TSHS) | SOKO LA AWALI (KG) | THAMANI SOKO LA AWALI (TSHS) | ZILIZOBANGULIWA (KG) | | THAMANI UWIANO WA GHAFI (TSHS) |
| | | | | | | | ZILIZOBANGULIWA | UWIANO WA GHAFI | |
| 1 | MTWARA | TANECU | 33,518,494.00 | 63,447,865,104.00 | 1,486,294.00 | 2,411,476,400.00 | 810,099.00 | 3,645,445.50 | 5,468,168,250.00 |
| | | MAMCU | 59,609,667.00 | 111,449,764,229.00 | 915,846.00 | 1,546,114,200.00 | 116,881.00 | 525,964.50 | 788,946,750.00 |
| 2 | LINDI | RUNALI | 42,440,859.00 | 81,187,464,564.00 | 7,200.00 | 11,520,000.00 | 2,611.00 | 11,749.50 | 17,624,250.00 |
| | | LINDI MWAMBAO | 14,622,801.00 | 25,590,331,828.00 | 487,780.00 | 848,494,500.00 | 195,454.00 | 879,543.00 | 1,319,314,500.00 |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 15,156,209.00 | 26,809,585,960.00 | 26,480.00 | 45,016,000.00 | | - | - |
| 4 | PWANI | CORECU | 10,759,505.00 | 18,796,294,846.00 | 1,415,619.00 | 2,468,173,500.00 | 269,043.00 | 1,210,693.50 | 1,816,040,250.00 |
| 5 | TANGA | TACACU | 339,519.00 | 569,336,325.00 | | | 6,521.00 | 29,344.50 | 44,016,750.00 |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | | | 18,769.00 | 30,968,850.00 | | - | - |
| 7 | MOROGORO | MOFACU | 153,959.00 | 264,846,120.00 | | | | - | - |
| 8 | TABORA | | | | 2,000.00 | 3,000,000.00 | | - | - |
| 9 | DODOMA | DOMASIKA | 24,079.00 | 40,164,540.00 | | | | - | - |
| 10 | MBEYA | TAMCU | 25,850.00 | 45,418,450.00 | 404.00 | 322,800.00 | | - | - |
| 11 | NJOMBE | TAMCU | 35,947.00 | 63,158,879.00 | | | | - | |
| 12 | KIGOMA | | | | 10,000.00 | 15,000,000.00 | | - | - |
| | JUMLA NDOGO | | 176,686,889.00 | 328,264,230,845.00 | 4,370,392.00 | 7,380,086,250.00 | 1,400,609.00 | 6,302,740.50 | 7,576,429,500.00 |
| | JUMLA KUU UZALISHAJI | | | | | | | | 187,360,021.50 |
| | JUMLA KUU THAMANI | | | | | | | | 343,220,746,595.00 |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

**NB**: Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023. Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea.

## Jedwali Na. 9b: Korosho Zilizouzwa Kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Machi, 2023) | | |
|---|---|---|
| KIPINDI CHA | KIASI KILICHOUZWA (KG) | THAMANI (TZS) |
| Mwezi Machi | 164,430 | 274,315,297 |
| Jumlishi Oktoba-Februari | 176,522,459 | 327,989,915,548 |
| Jumla | 176,686,889 | 328,264,230,845 |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

## Jedwali Na. 9c: Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Minada

| Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Mnada | | | |
|---|---|---|---|
| Mwezi Uliopita (Februari, 2023) | | Mwezi wa Sasa (Machi, 2023) | |
| Mwenendo wa Bei | Mwezi | Daraja la Kawaida | |
| | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,720 | 1,720 |
| | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,751 | 1,751 |
| | *Mabadiliko (%)* | ▼1.8% | ▼1.8% |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

## Jedwali Na. 9d Bei za Mauzo ya Korosho Ghafi Kimkoa.

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkoa (Machi, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | MWEZI | Daraja la Kawaida | |
| | | | Bei ya Juu | Bei ya Chini |
| MTWARA | MAMCU | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,705 | 1,680 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| | TANECU | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,605 | 1,604 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| LINDI | RUNALI | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,770 | 1,600 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| | LINDI MWAMBAO | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,726 | 1,726 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| PWANI | CORECU | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,520 | 1,520 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| RUVUMA | TAMCU | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,605 | 1,605 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| MOROGORO | MOFACU | *Bei ya Mwezi Machi* | NA | NA |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,721 | 1,721 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |
| TANGA | TACACU | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,719 | 1,719 |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | 1,751 | 1,751 |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | ▼1.8% | ▼1.8% |
| DODOMA | DOMASIKA | *Bei ya Mwezi Machi* | 1,719 | 1,719 |
| | | *Bei ya Mwezi Februari* | NA | NA |
| | | ***Mabadiliko** (%)* | | |

**Ufunguo: NA = HAIPO**

Alama (▲▼►) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei. (▲) Bei imeongezeka; (▼) Bei imeshuka; (►) Hakuna mabadiliko ya bei.

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania

## 4.1 TAARIFA YA MINADA KWA MIKOA YA TANGA, DODOMA NA SINGIDA

Msimu wa mavuno kwa mikoa ya kanda ya kati (Singida na Dodoma) na Kaskazini (Tanga) ikiwa ndio umeanza ambapo matarajio ya uzalishaji ni tani 2,000 kwa mkoa wa Tanga, tani 200 kwa mkoa wa Singida na tani 60 kwa mkoa wa Dodoma.

Mpaka sasa mkoa wa Tanga tayari umeshafanya minada miwili Mnada wa kwanza ulifanyika tarehe mosi mwezi Februari ambapo jumla ya kilo 199,168 ziliuzwa. Daraja la kwanza kilo 160,432 ziliuzwa kwa bei ya shilingi 1,751 kwa kilo na daraja la pili kilo

38,736 ziliuzwa kwa bei ya shilingi 1,401 kwa kilo. Mnada wa pili ulifanyika tarehe 11 Machi, 2023 ambapo jumla ya kilo 140,351 ziliuzwa, daraja la kwanza kilo 116,563 kwa bei ya shilingi 1,719 na daraja la pili kilo 23,788 kwa bei ya shilingi 1,420 kwa kilo. Minada hiyo katika mkoa wa Tanga itaendelea hadi mwezi Aprili kulingana na upatikanaji wa korosho.

Kwa upande wa Mkoa wa Dodoma mnada wa kwanza ulifanyika tarehe 28 Machi, 2023 ambapo jumla kilo 24,079 ziliuzwa, daraja la kwanza kilo 20,679 kwa bei ya shilingi 1,720 kwa kilo na daraja la pili kilo 3,382 kwa bei ya Tsh.1,350 kwa kilo. Katika Mkoa wa Singida ukusanyaji wa korosho ghafi ghalani ndio umeanza. Mikoa mingine inayolima korosho kama vile Kigoma, Katavi, Songwe na Tabora uzalishaji bado ni mdogo na Bodi ya Korosho inaendelea na utaratibu wa kuwatafutia masoko.

## 5.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023

Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji korosho duniani, huku ikishika nafasi ya pili katika bara la Afrika na nafasi ya sita duniani kwa mujibu wa taarifa za African Cashew Alliance (2021). Bodi ya Korosho Tanzania inatarajia kuratibu mkutano wa kimataifa wa korosho nchini utakaoitwa “Tanzania International Cashew Conference” kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2023 hadi 14 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere.

Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha maendeleo ya zao la korosho kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika zao la korosho. Kupitia mkutano huo, inatarajiwa ushiriki wa wadau mbalimbali katika nyanja za utafiti, utengenezaji mashine za usindikaji, viwanda vya ubanguaji, wawekezaji na wadau muhimu katika tasnia ya korosho nchini. Mkutano huo utaenda sambamba na maonyesho ya bidhaa zitokanazo na zao la korosho na teknolojia mbalimbali zitumikazo katika usindikaji wa bidhaa za korosho.

## 6.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA KOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi tayari manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya wilaya Nanyamba na Halmashauri ya wilaya Tandahimba zimehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea na mpaka sasa jumla ya wakulima 58,159 wamefikiwa na kuhuishwa taarifa zao katika halmashauri hizo tatu kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho Kufikia Tarehe 31/03/2023.**

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Mtwara | 1,936.00 |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Mtwara | 15,790.00 |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya Nanyamba | 26,590.00 |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya Tandahimba | 13,843.00 |
| | **Jumla** | **58,159.00** |

## 7.0 TAARIFA YA MAPOKEZI YA PEMBEJEO ZA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2023/2024

Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo, mabomba na gunia katika zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2023/2024. Upokeaji wa Pembejeo tayari umeanza katika ghala za kukusanyia zilizopo Mtwara. Aidha, kutakuwa na vituo vingine vya kupokelea pembejeo katika Mikoa ya Pwani na Lindi.

**Pembejeo za Korosho katika Ghala za Kupokelea Pembejeo Mjini Mtwara Zikisubiri Kusambazwa Kwa Wakulima Msimu 2023/2024**



**Jedwali Na. 11: Mapokezi ya Viuatilifu na Mabomba Msimu wa 2023/2024 Kufikia Tarehe 31 Machi, 2023**

| TAARIFA YA MAPOKEZI YA VIUATILIFU NA MABOMBA MSIMU WA 2023/2024 HADI KUFIKIA 31/03/2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **MZABUNI** | **KIUATILIFU/PEMBEJEO** | **KIUATILIFU CHA MAJI (LITA)** | **SULPHUR YA UNGA (KG)** | **KISUMBUFU DHIBITIWA** |
| 1 | BENZ AGRO | INDAZOLE | 164,460.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | BENSVIL 5SC | 37,540.00 | | Ubwiri Unga |
| 2 | MERU | PACHA | 149,987.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | METAX | 200,000.00 | | Ubwiri Unga na Ugonjwa wa Blaiti |
| | | AGROZEB GOLD | 100,000.00 | | Ubwiri Unga |
| 3 | BAJUTA | SULPHUR | | 353,225.00 | Ubwiri Unga |
| **JUMLA** | | | **651,987.00** | **353,225.00** | |
| 4 | FAHAMU | MABOMBA (IDADI) | 2,000.00 | | Upuliziaji na Unyunyiziaji |
| | MERU | MABOMBA (IDADI) | 3,000.00 | | Upuliziaji na Unyunyiziaji |
| **JUMLA** | | | **5,000.00** | | |




**MAWASILIANO:**

**MKURUGENZI MKUU**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA**

**Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450**

**Barua pepe: info@cashew.go.tz**

**Tovuti: www.cashew.go.tz**